



*Taarifa kwa vyombo vya habari, 11 Oktoba, 2012*

### **DAWA BANDIA – ARV: Maswali zaidi yanahitaji majibu**

Sikika imefurahishwa na taarifa za Wizara ya Afya kuhusu hatua ambazo imechukua hadi sasa kufuatia sakata la dawa bandia za kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI. Hata hivyo taarifa ya wizara iliyotolewa na Waziri wa Afya ndugu Hussein Mwinyi imetuacha na maswali kadhaa kama ifuatavyo;

1. Tunakubaliana na hatua ya Wizara kusimamisha matumizi ya dawa hizo na kuzirudisha MSD dawa zilizokuwa bado kwenye vituo vya kutolea huduma. Je, zoezi na kukusanya dawa hizo limehusisha pia kukusanya dawa ambazo tayari zilikuwa mikononi mwa watumiaji? Tunaelewa kwamba baadhi ya watumiaji huwa na kiasi kikubwa cha dawa majumbani kwa tahadhari zitakapokosekana vituoni. Je, serikali imeweza kuwafikia watumiaji wote kuwapa elimu, kuwaomba msamaha, na kuwapatia ushauri wa kisaikolojia?

2. Tunakubaliana pia na hatua ya Wizara kupitia TFDA kusitisha uzalishaji wa dawa zote katika Kiwanda cha TPI Ltd hadi uchunguzi wa suala hili utakapokamilika. Hata hivyo, Wizara iwapatie wananchi maelezo ni namna gani imeziba pengo hilo la uzalishaji na kudhibiti bei ya dawa kwa walaji isiongezeke kutokana na upungufu kama utatokea.

3. Tumefurahishwa na taarifa kwamba Wizara imehakikisha kuwa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI zenye ubora unaotakiwa zinaendelea kupatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya kote nchini. Kwa kuwa dawa hizi zilikuwa zikizalishwa na kiwanda cha TPI peke yake hapa Tanzania, Wizara iweaeleze wananchi imepata vipi na wapi hizo dawa mbadala. Ziliagizwa lini, kiasi gani, zilifika lini, na zilisambazwa vituoni lini. Hili ni la muhimu ili kuinua imani kwa watumiaji wasiendeleo na hofu kisha kuacha kuzitumia.

4. Tunakubaliana na maagizo kwa Waganga Wakuu wa Mikoa (RMOs) na Wilaya (DMOs) kuimarisha Kamati za Dawa na Tiba (Medicines and Therapeutic Committees) katika vituo vya huduma za afya, ambazo zina majukumu ya kusimamia upokeaji, uhakiki wa ubora na matumizi sahihi ya dawa na vifaa tiba. Je, wajumbe wa kamati hizi walipatiwa mafunzo ya namna ya kutambua dawa halisi na bandia? Je, kuna mwongozo ulio wazi na rahisi kuufuata iwapo kamati fulani itagundua dawa bandia kati ya dawa walizopokea? Je, ni kweli kwamba katika kila kituo cha kutolea hizi huduma kuna kamati hai?

5. Tumefarijika sana na taarifa kwamba uchunguzi kupitia vyombo vya usalama unaendelea kuhusu suala hili kwa hatua zaidi za kisheria. Hata hivyo, taarifa za dawa na vifaa tiba bandia zimekuwa zikitolewa na watoa huduma kwa muda mrefu sasa. Itakuwa na tija zaidi kama uchunguzi huu ukiwa mpana aina ya dawa na vifaa tiba kadhaa ili kutumia fursa hii kutatua hili tatizo kwa ujumla. Pia, kwa kuwa sekta ya afya


ina wadau wengi wa kisera, italeta ufanisi zaidi kama wadau wote wakahusishwa katika huu uchunguzi ili kukuza uwazi na uwajibikaji pamoja na ushirikiano wa kutatua tatizo hili.

6. Tungependa kusikia kutoka kwa Wizara namna ambavyo imejipanga ili tatizo hili na mengine yanayofana yasije kurudua tena huko mbele. Haina tija kugundua dawa bandia wakati wananchi wameshakula. Ni bora kuwa na mfumo ambao unahakikisha hakuna dawa au vifaa tiba vinavyosambazwa kwa walaji kabla havijakaguliwa na kuhakiki ubora wake. Tusingependa kuendelea na huu utaratibu wa kushutuka na kustaajabu kwamba dawa ambazo tulikwisha kula zilikuwa bandia.

7. Tungependa kusikia kauli ya serikali namna ilivyojipanga kitaalamu kusaidia watumiaji wa dawa hizi kuhusu tatizo la usugu unaoweza kutokea kutokana na kula dawa hizo bandia. Wagonjwa na watoa huduma wameelimishwaje kutambua dalili za usugu wa dawa (kama utajitokeza) na namna watakavyokabiliana nao.

8. Mwisho, tungependa kusikia kauli ya serikali kuhusu fidia kwa wale ambao tayari walitumia dawa zilizokuwa bandia, kama watapata madhara ya dawa bandia kwa njia ya usugu, mlipuko wa magonjwa nyemelezi, au vifo.

Tunaitakia mafanikio Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, na wadau wake wa kisera, katika kazi njema waliyoianza.



Bw. Irenei Kiria

Mkurugenzi Mtendaji, Sikika, S. L. P 12183 Dar es Salaam,

Simu: +255 222 666355/57, Nukushi: 2668015, Barua pepe: [info@sikika.or.tz](mailto:info@sikika.or.tz), Tovuti: [www.sikika.or.tz](http://www.sikika.or.tz)